



**LOWELL PUBLIC SCHOOLS**  
Ofisi za Usimamizi wa Kati Henry J. Mroz  
155 Merrimack Street  
Lowell, MA 01852

Novemba 16, 2020

Wapenzi Wanafamilia wa Lowell Public Schools,

Tunapokaribia sikukuu ya Thanksgiving, ningependa kuwashukuru tena kwa subira, uwezo wa kubadili mipango kirahisi, na ushiriki wenu - na pia kuwapatia arifa nyingine kuhusu namna hali ipo kuhusu lini wanafunzi watakapoweza kurejea shuleni.

Kwa bahati mbaya, data ya COVID-19 hapa Lowell - na kote Massachusetts - yaendelea kwenda katika mkondo usiyofaa. Mwezi wa Oktoba, tulipofanya tangazo kwamba tunabadilisha mpango wetu wa mafunzo ya awali na kuubadili na mpango unaotekelawa sasa, idadi ya wastani ya maradhi ya kila siku katika watu 100,000 ulikuwa 16.4 na "asilimia ya watu waliokuwa na maradhi" (asilimia ya vipimo zilizopatikana kuwa na maradhi hapa Lowell) ulikuwa 3.29%. Mwezi mmoja baadaye, Lowell bado inazingatiwa kama jamii yenye hatari ya juu, hata kulingana na miongozo yaliyorejelewa ya Commonwealth. Kulingana na idadi za mwisho kabisa, viwango vya wastani vya maradhi vya kila siku vimeongezeka kuwa asilimia 42.1 na asilimia ya viwango vya maradhi sasa ni juu zaidi na imefikia 6.45%.

Kulingana na mienendo haya ya data ya kiafya, na kulinda kujitolea kwetu wa kupea kipaumbele usalama wa wanafunzi, wafanyakazi, na jamii yetu pana, **tutakuwa tukiendelea na mpango wetu wa sasa wa mafunzo ya mbali hadi angalau Januari 4. Wanafunzi katika madarasa yetu ya elimu maalum pekee ndiyo wataendelea na mafunzo ya kuhudhuria darasani.**

Tafadhali elewa kwamba uamuzi huu haukuchukuliwa kirahisi. Tunaelewa namna mwaka huu umekuwa wenye wasiwasi. Ingawa bado kuna wakati uliobaki katika kalenda kabla ya likizo la kipupwe ili data ya kiafya ianze kuboreka, kufuatia ushauri na Bodi la Kiafya la Lowell Board of Health, inaonekana kwamba badiliko kama hili halitawezekena. Wakati huu, haionekani kwamba tutaweza kuwarejesha wanafunzi zaidi kwa mafunzo ya kuhudhuria kabla ya Januari 4, na tungependa kuwapatia arifa mapema iwezekanavyo kuhusu maamuzi haya.

Tutaendelea kufanya kazi na Bodi la Afya la Lowell ili kufuata mwenendo wa data ya COVID-19 na tutakupatia arifa zozote tunapozingatia mpango wetu wa mafunzo.

Wakati huo huo, tafadhali kumbuka kuendelea itifaki za usalama zinazopunguza usambazaji wa COVID-19 - umbali wa kijamii, kuvaa barakoa, na kutokusanyika katika vikundi vikubwa. Kasi tunayoweza kuboresha idadi zetu za COVID-19 hapa Lowell, ndiyo kasi tunayoweza kuongeza idadi za wanafunzi shuleni mwetu.

Asante sana tena kwa subira, uwezo wa kubadili mipango kirahisi, na ushiriki wenu kati muda huu usiyojulikana awali.

Wako Mwaminifu,

A handwritten signature in black ink, appearing to read "Joel Boyd".

Dr. Joel D. Boyd  
Msimamizi Mkuu wa Mashule